

# MIFUMO YETU

Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI

TOLEO NA. 8

FEBRUARI 2019 — APRILI 2019



**PlanRep**  
iliyoboreshwa

**Kuongeza Ufanisi katika uandaaji wa Mipango  
na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa na  
Vituo vya Kutolea Huduma**



***Mkufunzi wa Kitaifa wa mfumo wa PlanRep na Mchumi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI Allan Bendera wakati wa mafunzo ya PlanRep iliyoboreshwa kwa mikao ya Ruvuma, Mtwara na Lindi (Picha: Jacqueline Sombe– PS3)***

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*“ Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani”*



**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**



# Bodi ya Uhariri

## **Mwenyekiti**

*Mhandisi Joseph M. Nyamhanga  
Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## **Wajumbe**

*Erick Kitali – TAMISEMI  
Rebecca Kwandu – TAMISEMI  
Desderi Wengaa – PS3*

## **Waandishi**

*Sekela Mwasubila- Kondo Mji  
Fina Maziku – PS3  
Gladys Mkuchu – PS3*

## **Mhariri Mkuu**

*Angela Msimbira – TAMISEMI*

## **Wahariri**

*Erick Kitali – TAMISEMI  
Ntengejwa Hosseah– TAMISEMI  
Desderi Wengaa – PS3  
Gemini Mtei – PS3  
Conrad Mbuya – PS3*

## **Msanifu Kurasa**

*Jacqueline Sombe – PS3*

## **Jarida hili hutolewa na:**

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI  
S.L.P. 1923  
Dodoma-Tanzania  
Simu: (+255) 26 -2321234  
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz  
Tovuti: www.tamisemi.go.tz  
Blogu: blog.tamisemi.go.tz  
Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI  
Instagram: ortamisemi*

## **Ndani ya Jarida Hili:**

**Tahariri.....uk 6**

**PlanRep iliyoboreshwa kuwa Endelevu.....uk 7**

**PlanRep Yawezesha DFF Kufikia Malengo.....uk 8**

**Uboreshaji wa PlanRep Wapunguza Gharama za uandaaji wa bajeti Kondo Mji .....uk 9**

**Muungano Gateway kurahisisha utendaji wa PlanRep, Epicor na FFARS.....uk 11**

**TAHARIRI:**

## PlanRep Iliyoboreshwa

PlanRep iliyoboreshwa ni mfumo unaotumika katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na katika kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vituo vya kutolea huduma. Maboresho yanayofanywa mara kwa mara kwenye mfumo huu kwa ushirikiano wa OR TAMISEMI na mradi wa PS3 yamekuwa na tija sana katika kuboresha mipango na bajeti pamoja na utoaji ripoti/taarifa.

Mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa unaendelea kuongeza wigo wake wa matumizi ambapo humrahisishia kazi mtumiaji kutokana na ufanisi wa hali ya juu wa mfumo huu. Watumiaji wanaweza kuziona taarifa za watumiaji wengine ndani ya mfumo, jambo ambalo huwawezesha kujihakiki.

PlanRep imewezeshwa kuwasiliana na mifumo mingine kupitia Muungano Gateway ambapo tunaona mfumo huu utatumika kwenye sekta zote za Umma kwa kuunganishwa na mifumo mingine kusaidia kuboresha usimamizi na kuwezesha Serikali katika ngazi zote katika kutekeleza vizuri majukumu yake ya kutoa huduma.

Katika kuhakikisha uimarishwaji wa mfumo wa PlanRep unakuwa ni endelevu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, OR-TAMISEMI inaendelea kuwajengea uwezo wataalam wake waliopo katika ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri ili kutoa msaada wa kiufundi pindi mtumiaji wa mfumo anapokwama.

OR-TAMISEMI kupitia wataalam wake itahakikisha kila Halmashauri inaanda bajeti na mipango yake kuendana na maboresho ya utumiaji wa taarifa mara kwa mara katika mfumo.

Mfumo wa mipango na bajeti unaowiana kuanzia ngazi ya vituo vya kutolea huduma mpaka Serikali Kuu, utasaidia mchakato mzima wa uandaaji na utekelezaji wa mipango na bajeti. Hii itasaidia kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji ili kuchochea utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Nawatakia usomaji mwema wa jarida hili.

**Mhandisi Joseph M. Nyamhanga**  
**Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI**

## PlanRep iliyoboreshwa kuwa Endelevu

Mfumo wa kuandaa Mipango na Bajeti za Serikali za Mitaa (PlanRep) ulioboreshwa unaendelea kuimarishwa ili kuweza kuwa endelevu na kuendana na maendeleo ya teknolojia.

Hivi karibuni yamefanyika maboresho mbalimbali ili kuwezesha mfumo huu kuwa endelevu na kubadilika kulingana na ukuaji wa teknolojia na uwepo wa wataalamu wa kutosha wenye uwezo wa kuhudumia mifumo na watumiaji wake.

OR TAMISEMI imefanikisha kuufanyia mfumo marekebisha na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

Kaimu Mku-rugenzi Msaidizi wa

Miundombinu ya TEHAMA, OR-TAMISEMI Haji Bamsi anafanua kuwa maboresho yanayoendelea kufanyika kwa ushirikiano kati ya OR-TAMISEMI na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) ni pamoja na kuwawezesha watumishi wa Halmashauri kuhamisha matumizi yaliyokadiriwa kwa shughuli moja kwenda nyingine ('Reallocation') moja kwa moja ndani ya Mfumo wa PlanRep kwa kuzingatia ukomo wa bajeti na Sheria ya Bajeti, jambo ambalo lilikuwa ni changamoto wakati Halmashauri zilipoanza matumizi ya mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa.

Anaendelea kueleza kuwa kwa sasa mfumo wa PlanRep umeboresha nyaraka zinazotumika kama rejea wakati wa

kupanga, kutekeleza na kutoa taarifa za mipango na bajeti za Halmashauri. Nyaraka hizi ni kama vile Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri (CCHP) na Mfumo wa Muda wa Kati wa Mapato na Matumizi (MTEF) ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 maboresho makubwa yalifanyika katika baadhi ya vifungu kwenye MTEF na vile vile itakuwa mara ya kwanza katika mfumo wa PlanRep,

zimeweza kufanya tathmini za muda wa kati za mapato na matumizi, kuja TAMISEMI ambazo zimehusisha wataalamu katika ngazi ya mkoa kabla ya kufika wizarani," anasema Bamsi.

Pamoja na MTEF, nyaraka zingine ambazo zimeboreshwa ni Mwongozo wa Utoaji Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa (CFR) na Mwongozo wa Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Shughuli za Maendeleo za Mamlaka za

Serikali za Mitaa (CDR) ili kuweza kuwiana na kuendana na miongozo ya bajeti ya Wizarata ya Fedha na Mipango.

Bamsi anasema, ili kuwa na mfumo imara ni lazima watumiaji kuweza kupata urahisi wa

kutumia na katika kuhakikisha hilo OR-TAMISEMI imeweza kufanya mafunzo kwa watumiaji wote wa mifumo katika ngazi zote ili kuwajengea uwezo katika matumizi ya mfumo huu. Vile vile nyenzo mbalimbali kama vile dawati la usaidizi mtandaoni na Video za kufundishia, zimeandaliwa ili zitumike kama rejea ya matumizi ya mfumo.

Bamsi anaendelea kueleza kwamba, "hapo awali changamoto zote zilizokuwa zikitokea wakati wa kutumia mfumo, watumiaji walileta changamoto hizo moja kwa moja OR-TAMISEMI sababu ndipo wataalamu walipo. Kwa sasa kuna dawati maalum la

**inaendelea uk. 9**



Wakufunzi wa Kitaifa wa PlanRep kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI na PS3 wakitoa maelekezo kwa baadhi ya maafisa wa Manispaa ya Kigoma Ujiji wakati wa mafunzo elekezi ya mfumo wa PlanRep.(Picha: PS3)

MTEF kufanyiwa tathmini.

*“Nyaraka hizi zilizoboreshwa zitasaidia kuhakikisha upangaji makini wa matumizi wenye kuzingatia vipaumbele ili kuepuka matumizi yasiyo na tija”*

Nyaraka hizi zilizoboreshwa zitasaidia kuhakikisha upangaji makini wa matumizi wenye kuzingatia vipaumbele ili kuepuka matumizi yasiyo na tija.

“Vile vile katika MTEF kumeundwa vigezo vya kufanya tathmini ambavyo vitatumika kote wakati wa mchakato wa mipango na bajeti. Halmashauri zote

## PlanRep Yawezesha DFF Kufikia Malengo

Katika kutekeleza azma ya kuboresha utoaji wa huduma za afya na elimu nchini, Serikali iliamua kuweka utaratibu wa kupeleka fedha moja kwa moja kwenye akaunti za vituo vya afya na shule za Serikali *Direct Facility Financing* (DFF). Mfumo wa PlanRep ndio mfumo unaotumika kuboresha utekezaji wa utaratibu wa kupeleka fedha moja kwa moja kwenye akaunti za benki za vituo vya kutolea huduma.

“Katika sekta ya Elimu, shule za Msingi na Sekondari zinapokea fedha za ruzuku kutoka Wizara ya Fedha na Mipango moja kwa moja kwenda kwenye akaunti zao, wakati katika Sekta ya Afya yaani vituo vya kutolea huduma za afya vikiwemo zahanati, vituo vya afya na hospitali za Halmashauri zinapokea fedha za mfuko wa pamoja wa afya (Health Basket Fund-HBF) moja kwa moja kutoka Hazina kwenenda kwenye akaunti zao,” anaeleza Dkt. Gemini Mtei, Kiongozi wa Timu ya Mifumo ya Fedha kutoka Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3),

Anaendelea kusema kuwa, fedha zinazotokana na matibabu ya wanachama wa bima za afya nchini, ambazo ni za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF), zinalipwa moja kwa moja kwenye akaunti za benki za vituo husika. Fedha hizi zinatumiwa na kusimamiwa kupitia mfumo wa ‘FFARS’, ambao ni mfumo wa Kihisibu na Utoaji wa Taarifa za Fedha kwenye



**Kiongozi wa Timu ya Mifumo ya Fedha kutoka Mradi wa PS3 akitoa mafunzo ya PlanRep iliyoboreshwa kwa Maafisa Mipango, Waganga Wakuu, wahasibu pamoja na maafisa TEHAMA kutoka Mikoa ya Mbeya na Rukwa Mkoani Mbeya (Picha; Maktaba)**

vituo vya kutolea huduma.

“Hata hivyo utaratibu wa kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na mashuleni (DFF) hauwezi kuleta matokeo yanayotarajiwa katika uboreshaji wa huduma za afya na elimu ikiwa hakuna utaratibu imara wa Uandaaji wa Mipango na Bajeti. Mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa umekuja kuziba pengo hili na hivyo kuweka utaratibu bora wa kuandaa mipango na bajeti za vituo vya kutolea huduma,” anaongeza Dkt. Mtei

Kupitia mfumo wa PlanRep, vituo huainisha vipaumbele vyao na matokeo ya utoaji huduma yanayotarajiwa (Service Output) pamoja na shughuli au afua zitakazotekelezwa ili kufikia matokeo hayo na kuandaa bajeti itakayotumika kutekeleza shughuli au afua hizo. Kupitia mfumo huu ambao ni wa Kiel-ektroniki, wasimamizi kwenye ngazi ya Halmashauri, Mkoa pamoja na TAMISEMI wanaweza kuhakiki mipango na bajeti ya vituo vyote nchini kwa gharama nafuu ili kujiridhisha kama mipango na bajeti inayoandaliwa na vituo kwa kutumia fedha za DFF inajibu vipaumbele

vilivyomo kwenye jamii na vipaumbele vya kitaifa kabla ya kuanza matumizi ya fedha hizi za DFF.

Mfumo wa PlanRep unatumika kutoa ripoti za utekezaji wa vipaumbele vya matumizi ya fedha za DFF vilivyoainishwa kwenye mipango na bajeti ya vituo. Kwa kuwa mfumo huu wa PlanRep umeunganishwa na mfumo wa FFARS kupitia ‘Muungano Gateway’, mfumo wa PlanRep unaweza kutoa kwa wakati mmoja, taarifa za utekezaji wa

shughuli mbalimbali pamoja na taarifa ya fedha za DFF zilizotumika katika utekezaji wa shughuli hizo; tofauti na kipindi cha nyuma ambapo taarifa za utekezaji na taarifa za fedha zilikuwa zikipatikana kutoka mifumo tofauti.

Dkt. Mtei anaongeza kuwa “Utaratibu huu wa kutoa taarifa za utekezaji na matumizi ya fedha kwa pamoja kupitia PlanRep unaiwezesha Serikali na wadau mbalimbali kufanya tathmini ya thamani ya fedha ‘Value for Money’ zinazoenda kwenye vituo vya kutolea huduma. Taarifa za utekezaji na fedha kutoka PlanRep zinaiwezesha Serikali kufanya mrejesho kwa wadau mbalimbali na pia hutumika kufanya maboresho mbalimbali kwenye utaratibu mzima wa DFF.”

Kwa ujumla, mfumo wa PlanRep unawezesha kuhakikisha kwamba fedha za DFF zinatumiwa kutokana na malengo yanayotarajiwa na kupunguza au kuzuia kabisa matumizi ya fedha yasiyoridhisha.

**Na Mwandishi Wetu**



## PlanRep Iliyoboreshwa.....

### Inatoka uk 7

kushughulikia changamoto mbalimbali na dawati hili linaendelea kuboreshwa ambapo mpaka sasa changamoto zitakuwa zikitatuliwa kufuatana na muundo uliopo wa watumiaji na wataalamu kuanzia ngazi ya chini mpaka kufikia ngazi ya Wizara. Katika vituo vya kutolea huduma changamoto zao zitatatuliwa kwenye ngazi ya Halmashauri na iwapo itashindikana kutatuliwa zitapelekwa ngazi ya Mkoa hadi kufikia ngazi ya OR-TAMISEMI”.

Dawati maalum la msaada linafuata mfumo maalumu ambao changamoto ikiletwa na mtumiaji, atapatiwa tiketi maalumu yenye namba kutoka kwa Meneja wa Dawati la Msaada na atakabidhiwa mtaalam kuweza kushughulikia. Hii inarahisisha kufanya ufuatiliaji kwa kuwa tiketi ina namba maalum na itaweza kuwawajibisha wataalam kama changamoto hazitafanyiwa kazi kwa wakati. “Aidha tunaamini wataalam ndani ya Ofisi ya Rais TAMISEMI wako imara na wanaweza

kuwajengea uwezo wataalamu wengine zaidi katika kutumia mfumo huu kwakuwa lengo ni kuufanya kuwa endelevu na unaoenda na wakati kadri teknolojia inavyokuwa. Hivyo Serikali itaendelea kuwajengea uwezo wataalamu katika ngazi mbalimbali na hakikisha mfumo unakuwa imara,” anasisitiza Bamsi.

**Gladys Mkuchu- PS3**

## Uboreshaji wa PlanRep Wapunguza Gharama za Uandaaji Bajeti Kondoza Mji

Mfumo uliyoboreshwa wa kuandaa Mpango wa bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa (PlanRep) umeanza kutumika rasmi katika maandalizi ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kuwapatia mafunzo wataalam mbalimbali kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Halmashauri ya Mji wa Kondoza ni moja ya Halmashauri ambazo inatumia mfumo wa PlanRep katika maandalizi ya bajeti zake zote mbili yaani bajeti ya 2018/19 na bajeti ya 2019/20.

Mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa huanzia katika ngazi ya Halmashauri kupitia Idara ya Mipango ambayo kazi yake kubwa ni kuratibu zoezi zima la maandalizi ya bajeti kwa kuingiza vyanzo vyote vya mapato katika mfumo na kugawa fedha kwa kila Idara kulingana na ukomo wa bajeti.

Akifafanua zaidi kuhusu jukumu la Idara ya Mipango, Afisa Mipango wa Halmashauri ya Mji wa Kondoza Kaunga Amani anaeleza

“Kazi kubwa ya Idara ya Mipango ni kuandaa miongozo itakayotumika katika maandalizi ya bajeti ambayo itatumiwa na kila idara kwa kufuata mpango mkakati wa Halmashauri ambapo kila Idara itachukua malengo husika ambayo yanafuata dira na muelekeo wa Halmashauri” Anafafanua Amani.

Amani aliendelea kuelezea kuwa mfumo wa PlanRep uliyoboreshwa upo kimtandao lengo likiwa kupunguza gharama za uandaaji bajeti na kuweka viunganishi kuanzia ngazi ya chini kabisa hadi Wizarani.

Anasema mfumo wa PlanRep ili-

yoboreshwa umesaidia sana kufanya bajeti kuwa shirikishi kwasababu kila Mkuu wa Idara anashiriki mwenyewe katika kupanga bajeti tofauti na zamani ambapo ilikuwa ikifanywa na watu wachache.

Naye Mweka Hazina wa Halmashauri ya Mji Kondoza Onesmo Mwonga anaeleza kuwa mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa umewasaidia kwa kuunganisha mifumo yote ya kifedha ya Uhasibu na utoaji taarifa katika ngazi ya mtoa huduma ujulikanao kama (Facilities Financial Accounting and Reporting System FFARS) na mfumo wa EPICOR 10.2. Hali hii inasaidia katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti katika ngazi zote.

**Inaendelea uk 10**

# Uboreshaji wa PlanRep Wapunguza Gharama.....

## Inatoka uk 9

“PlanRep imetusaidia katika ufuatiliaji wa bajeti na ime-rahisishia katika uingizaji wa bajeti za fedha zinazopatikana nje ya mfumo ambapo kwa sasa unaweza kufanya kazi hiyo popote ulipo tofauti na awali ambapo ulilazimika kwenda hadi Wizarani.” Anasema Mwonga

Mwoga alisema, mfumo wa PlanRep umewasaidia sana katika maandalizi ya taarifa za robo mwaka za fedha ambapo kwasasa wanazitoa moja kwa moja kwenye mfumo tofauti na awali walipokuwa wakiandaa kwa mfumo tofauti wa Excel. Mfumo wa PlanRep umetuwezesha kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

ya Utumishi na Utawala inajukumu kubwa katika mfumo wa PlanRep hasa katika uandaaji wa bajeti ya mishahara kwa kujaza fomu mbalimbali ambapo fomu hizo hujipiga mahesabu na baadaye kupata taarifa fupi ya bajeti ya mishahara, upandishaji vyeo na madaraja, kuonyesha wastaafu watarajiwa na ajira mpya tofauti na ilivyokuwa awali.

Anaongeza kuwa kuna fomu namba 9 ambayo ni Tange ya watumishi ambayo inatoa taarifa ya miaka mitatu mbele ukijaza inajaza mpaka mwisho na fomu F ya wastaafu ambayo ukijaza utaona wastaafu kwa mwaka unaokuja ni wangapi na mishahara yao itakuwa ni shilingi ngapi hivyo mfumo huo umeboresha na kuimarisha shughuli ya kuandaa bajeti ya mishahara.



**Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa wakiwa katika kikao cha kupitisha Randama ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20 katika ukumbi wa Halmashauri hiyo (Picha : Sekella Mwasubilla-Halmashauri ya Mji, Kondoa)**

“Mfumo wa PlanRep ulioboreshwa unadhibiti bajeti za ziada/mbadala ambayo inaenda kutekeleza kili-chopangwa kwenye bajeti kulingana na chanzo cha fedha hivyo kila mtu atalipwa kulingana na chanzo kili-chotengwa kama mapato mengineyo (Other Charges-OC), Fedha za Miradi ya Maendeleo na mapato ya ndani (Own Source).” Anasema Mwonga.

Wakati huohuo Afisa Utumishi na Utawala wa Halmashauri ya Mji Kondoa Lucy Timba alieleza kuwa Idara

Aidha Mfumo wa PlanRep umewasaidia sana katika kuokoa muda na gharama nyingi zilizokuwa zikitumika hapo awali katika kuandaa bajeti ikiwa ni pamoja na kuwaongezea uwezo wa kumiliki bajeti yao ambapo mfumo unawapa fursa ya kushiriki kuandaa bajeti zao toka awali.

## **Sekela Mwasubilla- Kondoa Mji**

## Muungano Gateway kurahisisha utendaji wa PlanRep, Epicor na FFARS

**M**uungano Gateway ni mfumo wa kielektroniki wa Serikali unaowezesha mifumo mingine kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwa kurahisisha makutano ya mawasiliano baina ya mifumo ya ndani ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI), Wizara za Kisekta na wadau wanaohitaji taarifa na takwimu mbalimbali.

OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), imeboresha matumizi ya mifumo hii mitatu (PlanRep, Epicor na FFARS) kwa kutengeneza mfumo wa **Muungano Gateway** Unaoiunganisha mifumo yote na kuboresha utendaji kazi wake.

Muungano Gateway ni mfumo wa Serikali unaowezesha mifumo mingine kuwasiliana, kubadilishana taarifa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji taarifa na takwimu ndani ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Wizara za Kisekta na kwa wadau mbalimbali wanaohitaji taarifa na takwimu hizo. OR-TAMISEMI na PS3 waliona kuwa mifumo inategemeana katika ufanyaji kazi, hivyo waliunda mfumo wa *Muungano Gateway* ili kurahisisha mawasiliano baina ya mifumo hiyo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu

*“Muungano Gateway ni mfumo wa Serikali unaowezesha mifumo mingine kuwasiliana, kubadilishana taarifa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji taarifa na takwimu ndani ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI), Wizara za Kisekta na kwa wadau mbalimbali wanaohitaji taarifa na takwimu hizo.”*



**Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu ya TEHAMA Ofisi ya Rais TAMISEMI Hajji Idd Bamsi wakati wa mahojiano juu ya utendaji kazi wa Muungano Gateway (Picha: Mroki Mroki- TSN)**

ya TEHAMA OR -TAMISEMI, Hajji Bamsi anasema kuwa, awali sehemu ya ripoti ilikuwa inakosekana kwa sababu taarifa za matumizi zilikuwa kwa njia ya kawaida (manually) ambapo taarifa nyingi zilikuwa zikipotea na kufanya watumishi kutumia muda mwingi katika kuaanda taarifa mbalimbali na kupunguza ufanisi katika kazi zao.

“OR-TAMISEMI ilianza kwa kuunganisha mfumo mmoja na mwingine (one to one integration) ambao ulikuwa na changamoto katika mawasiliano ya mifumo zaidi ya miwili, baadae kwa kushirikiana na mradi

wa (PS3) waliweza kuunganisha mifumo zaidi ya miwili kwa kupitia mfumo wa *Muungano Gateway* ambao husafirisha taarifa kwenye mifumo yote”Anafafanua Bamsi.

Anasema kupitia *Muungano Gateway*, kumekuwa na urahisi katika utunzaji na upatikanaji wa taarifa muhimu za umma ambapo mfumo wowote unaweza kujiunga katika *Muungano* huu.

“Kupitia *Muungano Gateway*, mifumo iliyopo kwenye vituo vya kutolea huduma kama mfumo wa (GoTHOMIS) uliopo kwenye vituo vya afya unaweza kuwasiliana na kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya afya kupitia mfumo wa HIM (*Health Information Mediator*) ambao umeunganishwa na mifumo ya afya kama vile mfumo wa usambazaji dawa (eLMIS), mfumo wa taarifa za afya (DHIS2) na mfumo wa madaidai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).” Anaeleza Bamsi

Bamsi anaendelea kusema kuwa *Muungano* huu unarahisisha utunzaji taarifa muhimu za kiafya kama takwimu za wagonjwa na dawa, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wake pale zinapohitajika kwa muda muafaka katika vituo vyote vya afya nchini vinavyotumia mifumo hiyo ya TEHAMA.

“OR-TAMISEMI tukitaka taarifa kutoka mfumo wa DHIS2 ambao upo wizara ya afya tuziweke kwenye mfumo wa *PlanRep* kwa kuangalia viupaumbele

## Muungano Gateway .....

katika magonjwa yaliyo na idadi kubwa ya wagonjwa ili kutengeneza afuwa zaidi tuta- zipata taarifa hizo moja kwa moja kutoka mfumo wa HIM kupitia *Muungano Gateway* kwa sababu mfumo wa DHIS2 umeungwa tayari kwenye HIM.” Anaelezea Bamsi


Anaendelea kufafanua kuwa, Muungano huo umeweza kusaidia kusambaza taarifa zilizoboreshwa kutoka mfumo moja kwenda mifumo mingine yenye uhitaji wa taarifa maalum kutoka sehemu moja na kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kupunguza gharama katika mchakato wa uandaaji wa mipango na bajeti kwa kutumia mfumo wa (PlanRep).

“*Muungano Gateway* inaweza kutoa taarifa kwa haraka kutoka mfumo mmoja kwenda kwenye mfumo mwingine kulingana na mahitaji ya mfumo husika.” Bamsi akielezea zaidi.

Bamsi anasema kuwa kwa sasa ni rahisi kusimamia matumizi ya fedha kupitia mfumo wa EPICOR, FFARS na PlanRep, kwa sababu kila wakati mtumishi anapofanya matumizi, taarifa za muamala hufika ngazi zote za Halmashauri, Mkoa hadi TAMISEMI kwa muda mfupi kupitia *Muungano Gateway*. Hivyo imekuwa rahisi katika kutathmini matumizi na kuzifanya Halmashauri sasa kupitia *Muungano gateway*, kuweza kufanya matumizi kulingana na bajeti na ukomo wa bajeti.

Meneja wa Mifumo kutoka PS3 Revocatus Mtesigwa, analeza kuwa ili halmashauri na vituo vya kutolea huduma vifanye matumizi lazima wawe na vifungu vya bajeti katika mifumo ya fedha. Hivyo ni lazima mfumo wa PlanRep ubadilishane taarifa za mipango na bajeti kwenye mifumo ya Epicor na FFARS.

Mtesigwa pia alianisha faida ya mfumo wa



PlanRep kuwa ni uwazi katika matumizi na usimamizi wa pesa za umma, ambapo kupitia mfumo wa *Muungano Gateway*, ni rahisi kujua pesa zilizoingia, zilizotumika, kiasi kilichopo na bakaa ya mwaka uliopita. Hii hurahisisha kujua mchakato mzima wa matumizi na nukuu za taarifa za kiuhasibu ambazo hutumika katika ripoti.

Mtesigwa anasema mawasiliano baina ya mifumo hii ya TEHAMA, yamesaidia kudhibiti ubadhirifu wa pesa za umma na kuongeza mapato katika vituo vya afya. Kwa kuwa taarifa zote zipo wazi katika mifumo yote, nirahisi kupima na kutathmini utendaji, matumizi na maendeleo ya kituo au Halmashauri husika kupitia mifumo.

Serikali inampango wa kuboresha mifumo kwa kuunganisha mifumo mingine kwenye *Muungano Gateway* ifikapo mwaka 2020. Moja ya mifumo itakayo unganishwa ni mfumo wa (Epicor 9) wa Bohari ya Dawa

(MSD) ambao utarahisisha kusimamia na kufuatilia matumizi yote ya dawa yatakayofanyika na taarifa zake zitakuwa zinakwenda moja kwa moja kwenye mfumo wa FFARS kupitia *Muungano Gateway*.

Pia mfumo wa CBMS (*Central Based Management System*) ambao husimamia mipango na bajeti katika ngazi ya wizara na taasisi zilizo chini ya wizara ya fedha. Utaimarishwa kwa kuunganishwa na *Muungano Gateway* ili kuweza kupokea taarifa moja kwa moja kutoka PlanRep na kumrahisisha Waziri kuwasilisha mipango na bajeti ya Wizara, Mikoa na Halmashauri iliyopo katika PlanRep kupitia *Muungano Gateway* kwenda kwenye mfumo wa upangaji wa mipango na bajeti wa serikali kuu (CBMS).

**Fina Maziku- PS3**

